


WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA



TANGAZO KWA WANANCHI WA WILAYA YA MASASI

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya MASASI.; tunapenda kuwatangazia wananchi wote wenye umri wa miaka 18 na kuendelea wanaoishi Kata za Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kuanza kwa zoezi la Usajili na Utambuzi wa watu kwa lengo la kuwapatia Vitambulisho vya Taifa.

Kwa sasa zoezi linaendelea Kata ya MLINGULA NA NAMAJANI kuanzia tarehe 12/02/2018 jumatatu hadi tarehe 16/02/2018 ijumaa.

Wananchi mnakumbushwa kujitokeza kwa wakati. Vituo vinafunguliwa asubuhi saa 1.30 asubuhi hadi saa 10.30 jioni.

Zoezi hili linahusisha wananchi wote waliojiandikisha na kujaza fomu za usajili mwaka 2014 na wale ambao hawakuwahi kushiriki kabisa zoezi hili kwa maana ya waombaji wapya wenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

Kwa wale waombaji wapya, tunaomba mfike ofisi ya Serikali za Vijiji mnakoishi kujaza fomu za maombi ya Vitambulisho, kabla ya kuja kwenye kituo cha Usajili kuchukuliwa alama za vidole, picha na saini ya Kielektroniki. Na kwa wale waliojaza fomu za maombi ya usajili mwaka 2014 wafike kwenye vituo vya Usajili wakiwa na nakala (photocopy) ya viambatisho vyao mathalani kadi ya kupigia kura, cheti cha kuzaliwa, vyeti ya shule elimu ya msingi na sekondari, TIN namba, Kadi ya Bima ya Afya, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Leseni ya Udereva, Passport (Pasi ya kusafiria) na Kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi kama wewe ni Mzanzibari. Njoo na vile vyote ambavyo unavyo na kama huna kiambatisho chochote njoo na barua ya utambulisho.

Kusajiliwa kupata Kitambulisho cha Taifa kutakuwezesha kupata kwa haraka na kwa urahisi pembejeo za kilimo, ruzuku ya pembejeo, huduma za kijamii kirahisi mathalani huduma za afya, kupata mikopo katika taasisi za fedha na benki, kutambulika kirahisi kupata misaada pale inapohitajika, kusajili namba yako ya simu, kujidhamini au kudhamini na huduma nyinginezo nyingi. Zoezi ni bure.

VITUO VYA USAJILI VITAKUA KAMA IFUATAVYO

Kata ya MLINGULA Vituo vya kupigia picha vipo

1. KITUO :OFISI YA KATA MLINGULA (KWA KIJJI CHA MLINGULA NA MASIKU)
2. KITUO :OFISI YA KIJJI CHIKOWETI (KWA KIJJI CHA CHIKOWETI NA NAMBAYA)
3. KITUO: OFISI YA KIJJI NAMICHI (KWA KIJJI CHA NAMICHI)

Kata ya NAMAJANI Vituo vya kupigia picha vipo

1. KITUO:OFISI YA KATA NAMAJANI (KWA KIJJI CHA NAMAJANI, NAMAHINGA NA NGALOLE)
2. KITUO:OFISI YA KIJJI AMANI CHIRORO (KWA KIJJI CHA AMANI CHIRORO NA MIGOMBANI)

Kwa muonekano mzuri wa picha unashauriwa unapokuja kwenye kituo cha Usajili usivae nguo nyeupe, kijivu , bluu mpauko ,pinkii, nguo za kung'aa, jezi, nguo zenye nembo , kofia aina yoyote au kupaka hina mikononi.

Jitokeze leo usingoje kesho. Kata zitazofuata ni NAMATUTWE na MSIKISI, ratiba kamili mtatangaziwa hapo baadae. Ukisikia Tangazo hili mjulishe na mwenzako.

Limetolewa na Uongozi wa Wilaya kwa kushirikiana na NIDA